**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA (TPHPA)**

TPHPA

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

**01 Agosti, 2025 – Arusha**

# TAARIFA KWA UMMA

## Makampuni kumi na sita (16) ya Tanzania yapewa Usajili wa GACC Kusafirisha Parachichi kwenda China

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayofuraha kuutaarifu Umma wa Watanzania kwamba Makampuni kumi na sita (16) ya Parachichi za Tanzania yamepata usajili rasmi kutoka kwa Mamlaka ya Forodha ya China (GACC), ili kuanza kusafirisha Parachichi za Tanzania kwenda kwenye soko la China.

Usajili huu wa GACC umekamilika baada ya majadiliano ya uwili na mchakato wa ukaguzi wa mashamba na sehemu za kufungashia kufanyika kikamilifu na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, kuthibitisha kwambaTanzania sasa inakidhi mahitaji ya soko la China ya kuingiza bidhaa hiyo nchini humo. Kutokana na hali hiyo, wakulima wengi zaidi na Makampuni zaidi ya Parachichi sasa wanaweza kupeleka Parachichi katika soko la China, jambo ambalo linafungua fursa mpya ya biashara, kuongeza thamani na kuongeza kipato kwa Wakulima na Wafanyabiashara wa zao la Parachichi na hivyo kuchangia katika ukuaji wa Uchumi wa Tanzani.

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), inaendelea kuimarisha huduma zake kwa Wazalishaji na Wasafirishaji wa mazao nje ya nchi na kuhakikisha kunakuwa na ukuaji endelevu na wenye ushindani wa sekta ya mazao ya matunda na bustani. Tunawahimiza Wasafirishaji kuendelea kufuata viwango na matakwa ya masoko ya kimataifa ili kudumisha uadilifu, usafi wa mimea na uendelevu wa mauzo ya mazao ya bustani ya Tanzania nje ya nchi.

**Orodha ya Makampuni yaliyopata usaji wa GACC kusafirisha Parachichi ni kama Ifuatavyo:-**

1. Green Fruits Supplies Company Limited
2. Vegpro Tanzania Limited
3. Jamboo Fresh Limited
4. Tanzanice Agrofoods Company Limited
5. Tova Farm Company Limited
6. Seasons Orchards Ltd
7. Agrocert Tanzania Company Limited

Scanned with CamScanner

8. Avo Distribution Group Ltd
9. Lima Limited
10. Korongo 3 Agribusiness Ltd
11. Kibidula Farm Limited
12. Africado Limited
13. Avoafrica Tz Limted
14. Kuza Africa Company Ltd
15. Parachichi Fresh Products Ltd
16. USA Limited

Imetolewa na,

Prof. Joseph C. Ndunguru
**MKURUGENZI MKUU**
**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA (TPHPA)**

Scanned with CamScanner